

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

anwani ya simu
"Admin" BAGAMOYO"
Simu ya Mdomo: 023-2440002:
Fax No: 023-244009
Unapojibu tafadhali taja:
Kumb.Na.CAB.24/250/01/86



Ofisi ya Mkuu wa Wilaya
6 Mtaa wa Mkuu wa Wilaya
S.L.P 54'
61320 BAGAMOYO

18 JULAI, 2022

**TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI WA MAKARANI WA SENSE,
WASIMAMIZI WA MAUDHUI NA WASIMAMIZI WA TEHAMA.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze anawatangazia waombaji wa nafasi za kazi za muda za **Makarani, Wasimamizi wa Maudhui na Wasimamizi wa Tehama** kupitia tangazo la tarehe 05 Mei 2022 lililotolewa kwenye mtandao wa www.ajira.nbs.go.tz na www.tamisemi.go.tz Kuwa wamechanguliwa kuhudhuria usaili.

Kwa nafasi ya **Makarani wa sense na Wasimamizi wa Maudhui** usaili utafanyika ngazi ya kata katika Ofisi za Kata na **Wasimamizi wa Tehama** usaili utafanyika Makao makuu ya Halmashauri ya Chalinze.


Usaili wa nafasi zote utafanyika siku ya tarehe 20 Julai 2022 katika ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kata uliyoombea kuanzia saa 2:00 Asubuhi.

Waombaji wote wanatakiwa kufika na;

1. Vyeti halisi vyote (Original Certificates) vya Elimu na Taaluma kama vilivyoambatanishwa wakati wa kuomba ajira.
2. Cheti halisi cha kuzaliwa (Original Birth certificate)
3. Kitambulisho kwa ajili ya Utambuzi, Vitambulisho vinavyokubalika ni Kitambulisho cha Mkazi, Kitambulisho cha mpiga kura, kitambulisho cha Uraia, Leseni ya Udereva, Kitambulisho cha Nida na Hati ya kusafiria.
4. Fomu aliyotumia kuomba kazi kwenye mfumo kwa wale ambao hawajawasilisha fomu hizo kwa Watendaji wa Kata.

Waombaji wote ambao majina yao hayajaonekana katika Tangazo hili watambue kuwa maombi yao hayajafanikiwa.

Imetolewa na


Zainab Abdallah Issa
Mkuu wa Wilaya
BAGAMOYO

